JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SHERIA YA MTOTO

[SURA YA 13]

# TAFSIRI YA KANUNI ZA VITUO VYA KULELEA WATOTO WADOGO MCHANA NA WATOTO WACHANGA ZA MWAKA 2012

Toleo hili la Kanuni za Vituo Vya Kulelea Watoto Wadogo Mchana na Watoto Wachanga za mwaka 2014, Tangazo la Serikali Na. 147 la tarehe …….. mwaka 2012, ni Tafsiri Rasmi iliyosanifiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuchapishwa kwa mujibu wa kifungu cha 84 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Mbalimbali, Sura ya 1.

Dar es Salaam
28 April, 2016

GEORGE M. MASAJU,
*Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 167 la tarehe 13/05/2016

SHERIA YA MTOTO
(SURA YA 13)

———

KANUNI ZA VITUO VYA KULELEA WATOTO WADOGO MCHANA NA WATOTO WACHANGA ZA MWAKA 2014

MPANGILIO WA KANUNI

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Tarehe ya kuanza kutumika.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
MAOMBI YA USAJILI WA VITUO VYA KULELEA WATOTO WADOGO MCHANA NA WATOTO WACHANGA

4. Maombi ya usajili wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga.
5. Fomu ya maombi ya usajili wa jengo.
6. Uthibitisho wa uwezo wa kifedha na raslimali watu.

SEHEMU YA TATU
USIMAMIZI WA VITUO VYA KULEA WATOTO WADOGO NA WATOTO WACHANGA WASIOZIDI KUMI

7. Kamati ya wazazi.
8. Kanuni za ulinzi kwa watoto.
9. Taratibu za ulinzi kwa watoto.
10. Mahitaji ya watumishi na upekuzi.
11. Sifa za waangalizi wa watoto.
12. Masharti kuhusu watumishi walio zamu.
13. Kanuni za Maadili.

14. Jukumu la kutunza kumbukumbu.
15. Majalada binafsi.
16. Faragha na utunzaji siri.
17. Ada.

SEHEMU YA NNE
VIWANGO KWA AJILI YA MIUNDOMBINU YA VITUO VYA KULELEA WATOTO WADOGO MCHANA NA WATOTO WACHANGA

18. Mpangilio na ujenzi wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na watoto wachanga.
19. Usafi wa Mazingira.

SEHEMU YA TANO
VIFAA VYA KUCHEZEA NA HUDUMA

20. Wanasesere.
21. Vifaa vya burudani.
22. Chakula na lishe.
23. Vifaa kwa watoto walio chini ya miaka miwili.
24. Usalama.

SEHEMU YA SITA
UKAGUZI

25. Ukaguzi wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na watoto wachanga.

SEHEMU YA SABA
MASHARTI YA JUMLA

26. Rejesta ya vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na watoto wachanga.
27. Taarifa za robo mwaka na za mwaka mzima.
28. Muda wa kufungua vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na watoto wachanga.
29. Vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na watoto wachanga vya jamii.
30. Kufutwa kwa Kanuni.

---

MAJEDWALI

---

## SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1.** Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Vituo vya kulea Watoto wadogo mchana na watoto wachanga za mwaka 2014.

Tarehe ya kuanza kutumika

**2.** Bila kujali kifungu cha 154 cha Sheria, Kanuni hizi zitaanza kutumika katika tarehe zitakapochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, isipokuwa kwa Sehemu za III, IV na V zitaanza kutumika miezi ishirini na nne baada ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi.

Tafsiri

**3**. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mtoto;

Sura 13

"afisa aliyeidhinishwa" maana yake ni Afisa Ustawi wa Jamii au Afisa afya, kama itakavyokuwa, ambaye ni kiongozi wa eneo lililoteuliwa;

"mlezi wa mtoto" maana yake ni mtu mwenye cheti cha shule ya sekondari na cheti cha malezi ya awali na maendeleo ya mtoto au sifa nyingine stahiki kutoka katika taasisi inayotambulika aliyeajiriwa na kituo cha kulelea watoto wadogo na mchana au kituo cha watoto wachanga kwa ajili ya kutoa uangalizi wa karibu kama mzazi, usimamizi na mwongozo kwa watoto kwenye taasisi;

"usalama wa mtoto" maana yake ni vitendo vyote vinavyolenga kumlinda na kuzuia udhalilishaji, ukatili, unyanyasaji na utelekezwaji wa mtoto;

"masuala ya usalama wa mtoto" maana yake ni hisia, taarifa, tuhuma na utoaji taarifa zinazohusu udhalilishaji, ukatili, unyanyasaji au utelekezaji watoto;

"kanuni za maadili" maana yake ni kanuni zinazopaswa kuzingatiwa na wafanyakazi, watu wengine au Kamati;

"Kamishna" maana yake ni Kamishana wa Ustawi wa Jamii;

"Idara" maana yake ni Idara ya Ustawi wa Jamii;

"ulemavu" maana yake ni hali inayotokana na dosari kwenye mwili, akili na milango ya fahamu ambayo inasababisha mtu kushindwa kutenda mambo ambayo kwa kawaida angetegemewa kuiyaweza na hivyo kumletea mtu huyo

kizuizi katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku.

“vifaa vya kuzimia moto” ni pamoja na vifaa vya kuzimia moto, ndoo za mchanga na mablanketi maalum pamoja na vifaa vingine vinavyopatikana kwenye mazingira husika.

“Afisa Afya” maana yake ni afisa katika utumishi wa Serikali au taasisi ya kitabibu iliyosajiliwa;

“taasisi” haijumuishi shule ya maadilisho, mahabusu, makao ya watoto, malezia yaliyoidhinishwa au vituo vya maafa;

“watoto walio kwenye mazingira hatarishi zaidi” maana yake ni mtoto anayehitaji uangalizi na ulinzi kama ilivyotamkwa kwenye kifungu cha 16 cha Sheria, watoto wanaokinzana au walio katika hatari ya kukinzana na sheria na watoto wenye ulemavu;

“yatima” maana yake ni mtoto aliye chini ya umri wa miaka 18 ambaye amepoteza mzazi mmoja au wote wawili;

“majengo” maana yake ni eneo ambalo kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga wasiozidi kumi kinaendeshwa;

“kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga cha mtu binafsi” inarejea kituo cha kulelea watoto wadogo mchana na watoto wachanga kinaendeshwa na mtu binafsi au kampuni;

“kituo cha kulea watoto wachanga” maana yake ni kituo cha kulea watoto wachanga au watoto wachanga wasiozidi kumi kinachoendeshwa na mamlaka za serikali za mitaa au chombokingine cha Serikali;

“Afisa Ustawi wa Jamii” maana yake ni Afisa Ustawi wa Jamii wa Jiji, Wilaya, Halmashauri au Manispaa kwa kadri itakavyokuwa;

“mgeni” maana yake ni mtu yeyote asiye mwajiriwa au mfanyakazi wa kawaida wa kituo cha kulelea watoto wadogo au watoto wachanga.

## SEHEMU YA PILI
### MAOMBI YA USAJILI WA VITUO VYA KULELEA WATOTO WADOGO MCHANA NA WATOTO WACHANGA

Maombi ya usajili wa

**4.**-(1) Mtu hataendesha kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga isipokuwa kama anamiliki cheti

kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga

halali cha usajili kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

(2) Mtu mwenye akili timamu au taasisi ambayo haijatangazwa kuwa mufilisi au ambayo haitakiwi, kwa mujibu wa Sheria za Tanzania, inaweza kuomba usajili wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga.

(3) Cheti cha usajili hakitatolewa chini ya Kanuni hizi isipokuwa kama Afisa Afya wa eneo ambalo kituo husika ambako kituo cha kulea watoto wachanga au watoto wachanga wasiozidi kumi kitaanzishwa, amekagua na kupendekeza kwamba jengo husika linafaa kwa kuanzisha kituo cha kulea watoto wachanga au watoto wachanga wasiozidi kumi.

(4) Cheti cha usajili hakitatolewa chini ya Kanuni hizi kuhusiana na jengo lililopangishwa isipokuwa kama muda wa kupangisha ni wa kipindi si chini ya miaka mitatu na kwamba mkataba huo wa kupangisha jengo umesajiliwa na Msajili wa Hati.

(5) Mtu yeyote ambaye amepewa cheti cha usajili hatakodisha, pangisha, kuuza, kuhamisha au kwa namna yoyote ile kutoa cheti hicho kwa mtu mwingine bila taarifa ya maandishi kwa Kamishna, ambaye anaweza kuidhinisha maombi kwa wakati baada ya kujiridhisha kwamba matumizi hayo ya usajili ni halisi na hayataathiri malezi ya watoto.

(6) Kamishna hataidhinisha taarifa chini ya kanuni ndogo ya (5) isipokuwa-

(i) amejiridhisha kwamba usajili ni halisi; na

(ii) kwamba kukodisha huko, kupangisha, kuuza, kuhamisha au kutoa kwa namna nyingine cheti hicho hakutaathiri malezi ya mtoto.

Fomu ya maombi ya usajili wa jengo

**5**.-(1) Mtu mwenye nia ya kusajili-

(a) kituo cha kulea watoto wachanga atawasilisha maombi yake kwa Afisa Ustawi wa Jamii katika eneo ambalo kituo kipo na kwa kutumia Fomu Na. 1 kama ilivyowekwa kwenye Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi;

(b) kituo cha kulelea watoto wachanga atafanya maombi kwa Afisa Ustawi wa Jamii wa eneo ambalo kituo kipo kwa kutumia Fomu Na. 2 kama ilivyowekwa kwenye Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

(2) Afisa Ustawi wa Jamii, ndani ya siku arobaini na tano toka tarehe ya kupokea maombi-

(a) atapitia maombi husika; na

(b) atafanya uamuzi wa iwapo au la maombi husika yamekidhi vigezo vilivyoainishwa chini ya Sheria na Kanuni hizi; na

(c) atamtaarifu Afisa Afya kufanya ukaguzi stahiki wa majengo ya kituo.

(3) Afisa Afya atafanya ukaguzi kujiridhisha iwapo majengo husika yanafaa ndani ya siku ishirini na tano toka tarehe ya kupokea taarifa kutoka kwa Afisa Ustawi wa Jamii.

(4) Afisa Ustawi wa Jamii baada ya kupokea taarifa ya ukaguzi katika kanuni ndogo ya (5), atawasilisha maombi husika kwa Kamishna ili kupata kibali chake ndani ya siku kumi na nne.

(5) Pale ambapo Kamishna amejiridhisha kwamba maombi husika yamekidhi matakwa ya Kanuni hizi, atatoa cheti cha usajili kama iilivyowekwa kwenye Jedwali la Pili la Kanuni hizi ndani ya siku ishirini na moja toka tarehe ya kupokea maombi husika.

(6) Pale ambapo maombi hayajakidhi matakwa ya kanuni ndogo ya (2)(b), Afisa Ustawi wa Jamii atayakataa maombi hayo na kurudisha maombi husika kwa mwombaji ndani ya siku kumi na nne, na akiainisha sababu za kukataa fomu husika za maombi.

(7) Mwombaji ambaye maombi yake yamekataliwa na kurudishwa, anaweza kuwasilisha upya maombi yake baada ya kutimiza masharti yaliyoainishwa kwenye fomu iliyokataliwa.

(8) Mwombaji ambaye haridhishwi na uamuzi wa kukataliwa kwa maombi yake chini ya kanuni ndogo ya (4) atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Kamishna ndani ya siku thelathini toka tarehe ya kupokea taarifa ya kukataa maombi.

(9) Kamishna-

(a) atafanya marejeo ya rufaa;

(b) atatoa fursa kwa mwombaji kusikilizwa; na

(c) atatoa uamuzi juu ya rufaa ndani ya siku sitini toka tarehe ya kusikilizwa rufaa.

(10) Mtu yeyote ambaye haridhishwi na uamuzi wa Kamishna atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Waziri ndani ya siku thelathini toka tarehe ya kupokelewa taarifa ya uamuzi wa kukataa maombi kwa mujibu wa kifungu cha 156(c) cha Sheria.

(11) Uamuzi wa Waziri utakuwa ni wa mwisho.

(12) Endapo Waziri atakataa maombi, mwombaji atawasilisha maombi mapya baada ya kupita miezi kumi na mbili toka tarehe ya kuwasilisha maombi yaliyokataliwa

Uthibitisho wa uwezo wa kifedha na rasilimali watu

**6.-**(1) Cheti cha usajili kisitolewe isipokuwa kama mwombaji amewasilisha ushahidi wa-

(a) upatikanaji wa fedha za kutosha kama inavyoweza kuainishwa kwenye Mwongozo utakaotolewa na Kamishna, ndani ya miezi mitatu tangu tarehe ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi;

(b) uwezo wa kustahimili uendeshaji wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga; na

(c) taarifa ya benki kama uthibitisho mtiririko wa mapato na vyanzo vya mapato.

(2) Kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga ambacho kimesajiliwa kwa mujibu wa kanuni hizi hakitaanza kazi mpaka meneja au mmiliki awe ameajiri watumishi wanaohitajika ambao wamefanyiwa upekuzi kwa mujibu wa Kanuni hizi.

## SEHEMU YA TATU
### USIMAMIZI WA VITUO VYA KULELEA WATOTO WADOGO NA WATOTO WACHANGA WASIOZIDI KUMI

Kamati ya wazazi.

**7.-**(1) Kila kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga kitakuwa na kamati ya wazazi ambayo muundo wake utakuwa kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

(2) Majukumu ya kamati ya wazazi yatakuwa ni-

(a) kuandaa, kusaidia na kusimamia utekelezaji wa miradi na programu za kituo husika cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga wasiozidi kumi;

(b) kuandaa mipango endelevu na miradi yenye lengo la kuongeza pato la kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga ili kiweze kuboresha huduma zake na kuongeza fursa ya watoto kujiunga na kituo husika cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga wasiozidi kumi; na

(c) kushauri kuhusu masuala mengineyo kama

itakavyohitajika na Kamishna, meneja au mmiliki wa kituo husika cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga.

(2) Kamati ya wazazi itaandaa taarifa ya kila robo mwaka na kuiwasilisha kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji au Afisa Mtendaji wa Mtaa ambaye naye ataiwasilisha kwenye Halmashauri ya Kata kwa ajili ya kuwasilishwa Jiji, Wilayani, katika Halmshauri au kwa Afisa Ustawi wa Jamii wa Manispaa, kwa kadri itakavyokuwa.

Kanuni za ulinzi kwa watoto.

**8.-**(1) Mmiliki au meneja wa kituo cha kulea watoto wadogo mchana au watoto wachanga atahakikisha kwamba hatua za kiusalama na mikakati ya uwajibikaji ipo na inaainisha utaratibu wa kutoa taarifa kuhusu tuhuma na namna ya kushughulika na masuala yanayohusu usalama wa mtoto.

(2) Usalama wa mtoto utajengwa katika misingi ifuatayo-

(a) mtoto ana haki ya kulindwa dhidi ya madhara, kutelekezwa, udhalilishwaji na utumikishwaji wa kingono na aina nyingine yoyote ya udhalilishaji au ukatili, bila kujali jinsi yao, umri, dini, lugha, itikadi ya kisiasa, ulemavu, afya, lishe na hali ya kisaikolojia, utamaduni, asili yake, kwamba ametoka kijijini au mjini, kuzaliwa, hali yake ya kiuchumi na kijamii au kwamba yeye ni mkimbizi au ana hali nyingineyo; na

(b) maslahi bora ya mtoto.

(3) Kila mtu ana wajibu wa kutoa taarifa mara moja kuhusiana na suala lolote linalohusu usalama wa mtoto, hisia au utolewaji taarifa na kukiukwa kwa Kanuni za Maadili kwa mmiliki, meneja au mamlaka stahiki.

(4) Masuala ya usalama wa mtoto na tuhuma kuhusiana na ukiukwaji wa Kanuni za Maadili zitapewa uzito unaostahili na kushughulikiwa kwa wakati na kwa namna inayostahili.

(5) Ukatili, udhalilishaji, utumikishwaji na utelekezaji wa mtoto utakaofanywa na mtumishi wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana utachukuliwa kama ni kitendo cha ukiukwaji wa hali ya juu wa maadili ya kazi na itakuwa ni sababu ya kuchukuliwa hatua za kinidhamu, ikiwemo kufukuzwa kazi.

(6) Tuhuma za mwenendo unaopelekea kosa la jinai ni lazima zitakuwa taarifa kwenye mamlaka stahiki.

(7) Mtoto hataadhibiwa au kuathiriwa kwa namna yoyote

ile kwa kutoa tuhuma za kufanyiwa ukatili, kudhalilishwa, kutumikishwa au kutelekezwa.

(8) Mmiliki yeyote au meneja wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga atakuwa na wajibu wa kutoa mafunzo rahisi stadi za maisha kwa watoto kulingana na umri wao kwa ajili ya usalama wao dhidi ya udhalilishaji.

Taaratibu za ulinzi kwa watoto.

**9**.-(1) Mmiliki yeyote au meneja wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga atahakikisha kwamba hatua za kiusalama na mikakati ya kimwitikio inawekwa na ambayo inatoa utaratibu wa kutoa taarifa kuhusu tuhuma na utolewaji wa tuhuma dhidi ya mtoto na namna ya kushughulika na masuala ya usalama wa mtoto.

(2) Utaratibu wa usalama wa mtoto utahakikisha kwamba-

(a) tuhuma zinaripotiwa mara moja kwa meneja au mmiliki wa kituo cha kulea watoto wachanga au watoto wachanga wasiozidi kumi;

(b) upelelezi wa awali kuhusu tuhuma unafanywa ndani ya saa 24;

(c) mtoto, iwapo ana uwezo wa kuelewa suala husika, anataarifiwa kwa undani kuhusu utaratibu na haki yake ya kushiriki na kutoa maoni yake;

(d) mtoto anapewa misaada yote muhimu, ikiwemo huduma ya afya, ushauri na kuondolewa woga au mashaka;

(e) faragha ya malalamiko ya mtoto na utu wake vinalindwa;

(f) hatua za makusudi zinachukuliwa ili kuhakikisha usalama wa mtoto, ikiwemo, iwapo ni muhimu, kumsimamisha kazi kwa muda mtumishi wa kituo cha kulelea watoto wadogo au watoto wachanga ambaye tuhuma zimeelekezwa kwake na kumzuia asiingie kwenye eneo la kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga na kuonana na mtoto mlalamikaji, wakati upelelezi unaendelea;

(g) mtoto mlalamikaji, wazazi au mlezi, kwa kadri itakavyokuwa, wanataarifiwa kuhusu suala husika la usalama wa mtoto mapema iwezekanavyo na wataendelea kutaarifiwa kuhusu mwenendo wa

upelelezi;

(h) mienendo ya kinidhamu au kijinai inachukuliwa iwapo itaonekana inafaa; na

(i) mifuko yote inaongwa na na msingi wa "maslahi bora ya mtoto" kama kigezo cha msingi.

(3) Mmiliki yeyote au meneja wa kituo cha kulea watoto wachanga au watoto wachanga wasiozidi kumi atahakikisha kwamba watumishi wote, wazazi, walezi na wageni wanapata na kutaarifiwa kuhusu utaratibu wa kimaandishi wa usalama wa mtoto na kwamba mtoto mwenye uwezo wa kutosha wa kuelewa masuala ya msingi ya utaratibu wa usalama wa mtoto katika lugha inayofaa kulingana na umri wao.

Mahitaji ya watumishi na upekuzi

**10**.-(1) Meneja yeyote au mmiliki ataajiri idadi ya watumishi watakaojulikana kama "walezi wa watoto" na watumishi wengine wasaidizi kama vile wapishi, wafanya usafi, watunza bustani, walinzi na waangalizi kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu katika kituo cha kulelea watoto wachanga au watoto wachanga, kwa kuzingatia idadi, uwiano wa kijinsia, umri, hali ya kiafya na mahitaji ya mtoto anayehudhuria katika kituo husika cha kulelea watoto wadogo au watoto wachanga.

(2) Bila kujali kanuni ndogo ya (1), meneja au mmiliki atahakikisha kwamba kuna watumishi wa kutosha kwa kuzingatia kanuni ya 11(3) na kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

(3) Kila meneja au mmiliki mwenye nia ya kuajiri mtumishi kutoka nje ya nchi ili afanye kazi katika kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga anaweza kumwajiri mtumishi huyo kwa kuzingatia sheria yoyote ambayo kwa wakati huo inatumika kuhusiana na suala hilo.

(4) Meneja au mmiliki wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au wachanga atawasilisha kwa Kamishna majina ya watumishi wanaotarajiwa kuajiriwa pamoja na sifa zao.

(5) Kamishna au mtu aliyekasimiwa mamlaka kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa atapekua watumishi wote wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au wachanga au watoto wachanga ndani ya miezi mitatu kutoka tarehe ya kuwasilishwa kwa orodha ya majina ya watumishi wanaotarajiwa kuajiriwa.

(6) Pale ambapo upekuzi haukukamilika ndani ya mwezi

tangu jina au majina ya watumishi wapya yawasilishwe, mmiliki au meneja atakuwa na uhuru wa kuajiri watumishi hao wapya.

Sifa za waangalizi wa watoto

**11**. Mmiliki wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga hataajiri mtu kama mlezi wa mtoto ambaye-

(a) ana umri chini ya miaka 18;
(b) hajapata angalau cheti cha kuhitimu masomo ya sekondari ya kidato cha nne;
(c) hana cheti cha malezi makazi na maendeleo ya awali ya mtoto na maendeleo au sifa nyingineyo stahiki kutoka kwenye taasisi inayotambulika; na
(d) amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai.

Masharti kuhusu watumishi walio zamu

**12.**-(1) Mmiliki au meneja atahakikisha kwamba watumishi wa malezi ya watoto wenye sifa wanakuwepo zamu ili kutoa huduma za malezi na usimamizi kwa idadi ya watoto waliohudhuria katika kituo husika cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga.

(2) Idadi ya chini ya watumishi wa malezi wa zamu itajumuisha watumishi wa malezi ya watoto na waangalizi walioajiriwa kwa ajili ya kutoa uangalizi wa karibu kwa kusimamia na kuwapa mwongozo changamshi wa awali, kujifunza kwa vitendo na stadi za maisha kwa watoto walio katika kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga.

(3) Mwangalizi wa mtoto atatakiwa kuwa na uzoefu wa angalau miaka miwili katika kuwalea watoto.

(4) Mmiliki au meneja atahakikisha kwamba masuala yafuatayo kuhusiana na matunzo ya mtoto yanazingatiwa-

(a) mwangalizi wa mtoto kwa uwiano watoto ni kama iliyowekwa kwenye Jedwali la Nne la Kanuni hizi;
(b) watumishi waangalizi kwa uwiano wa mtoto ni kama inavyoainishwa kwenye Jedwali la Nne la Kanuni hizi;
(c) angalau wafanyakazi waangalizi wasiopungua watatu wapo zamu wakati wote, ikiwa ni pamoja na angalau mwangalizi wa mtoto mmoja kwa mtoto;
(d) upatikanaji wa mtumishi mmoja aliye na ujuzi wa huduma ya kwanza kwa wakati wote; na
(e) uwepo wa mtumishi mmoja mwenye ujuzi wa matumizi ya vifaa vya kuzimia moto kwa wakati wote.

(5) Pale ambapo kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga kinaandikisha mtoto mwenye ulemavu, maradhi sugu, utapiamlo au aliye na VVU/UKIMWI, mbali na mahitaji ya kiwango cha chini cha watumishi wa zamu chini ya kanuni ya 11(3) na Jedwali la Pili la Kanuni hizi, mmiliki au meneja atahakikisha kwamba kuna angalau watumishi wa malezi wa zamu kwa kila watoto watano.

(6) Mmiliki au meneja wa kituo cha kulelea watoto wadogo au watoto wachanga kumi atahakikisha kwamba kuna idadi ya kutosha ya watumishi wasaidizi wa zamu kwa ajili ya uendeshaji bora na usalama wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga.

(7) Bila ya kujali kanuni ndogo ya (6), watumishi au watoto walio na magonjwa ya kuambukiza hawatahudumiwa katika namna inayowanyanyapaa.

(8) Mmiliki au meneja atachukua hatua zote stahiki kuhakikisha kwamba watumishi au watoto wenye maradhi ya kuambukiza hawagusani na watoto wengine, kwa namna ambayo inaleta athari kwa wengine.

(9) Mmiliki au meneja atahakikisha kwamba-

(a) wafanyakazi wote, bila kujali vyeo vyao, wanapata mafunzo ya awali ambayo yatajumuisha mafunzo ya Kanuni zinazoongoza vituo vya kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga wasiozidi kumi, Kanuni za Maadili zilizo kwenye Jedwali la Tano na sera na taratibu za usalama wa mtoto;

(b) kuna mafunzo ya kazini ya mara kwa mara, ambayo yanaendana na cheo cha mfanyakazihusika na itajumuisha:

(i) ukuaji na maendeleo ya mtoto, msaada wa kisaikolojia na kijamii na utambuzi wa awali wa watoto wenye ulemavu na namna ya kushughulika nao;

(ii) mbinu za kudhibiti tabia;

(iii) unyeti wa masuala ya jinsia;

(iv) masuala ya usalama wa mtoto, ikiwemo utaratibu wa usalama wa mtoto na Kanuni za Maadili; na

(v) utunzaji wa kumbukumbu na usimamizi wa

masuala mbalimbali.

Kanuni za Maadili

**13**.-(1) Wafanyakazi wote wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga wajumbe wa Kamati ya Wazazi, wawakilishi wa mashirika au idara, taasisi binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali, taasisi za dini na watumishi wa kujitolea wanaotembelea kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga watatakiwa kufuata Kanuni za Maadili zilizoainishwa kwenye Jedwali la Tano la Kanuni hizi.

(2) Waziri anaweza kurekebisha Kanuni za Maadili iwapo anaona inafaa kufanya hivyo.

(3) Mmiliki au meneja atahakikisha kwamba nakala ya Kanuni za Maadili inawekwa kwenye sehemu inayoonekana na inayofikika kwa urahisi na watumishi na wageni wote.

(4) Itakuwa ni jambo la lazima kwa watumishi na wajumbe wote wa kamati ya wazazi kuweka saini katika Kanuni za Maadili.

Jukumu la kutunza kumbukumbu

**14.** Mmiliki yeyote au meneja wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga atatunza kumbukumbu zifuatazo:

(a) Rejesta ya kuandikisha Watoto;

(b) Rejesta ya Matukio ambamo ndani yake kila tukio muhimu linalohusiana na kituo cha kulea watoto wachanga au watoto wachanga wasiozidi kumi litarekodiwa;

(c) Rejesta ya Wageni ambayo ndani yake kutawekwa maelezo ya wageni wote waliotembelea kituo husika cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga;

(d) Rejesta ya Malalamiko, ambayo ndani yake kutarekodiwa malalamiko yote ya unyanyasaji wa watoto yaliyotolewa na watoto au na mtu yeyote na hatua zilizochukuliwa.

Majalada binafsi

**15**.-(1) Kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga kitatunza jalada binafsi kwa kila mtoto aliyeandikishwa.

(2) Kila jalada binafsi litakuwa na mambo yafuatayo:

(a) majina kamili ya mtoto yakiwemo majina yoyote ya

utani ya mtoto husika yanayofahamika;

(b) majina kamili na mawasiliano ya mzazi au mlezi wa mtoto;

(c) tarehe na mahali mtoto alipozaliwa;

(d) kabila la mtoto;

(e) jinsi ya mtoto;

(f) mahali mtoto anapoishi;

(g) dini, asili au mwelekeo wa kiutamaduni wa mtoto;

(h) taarifa kuhusu afya ya mtoto, ikiwemo aleji, taarifa kuhusu chanjo na uangalizi wowote wa kitabibu au matibabu yaliyofanyika kwa mtoto wakati akiwa kwenye kituo husika cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga;

(i) taarifa kuhusuulemavu wa kimwili au ulemavu mwingine wowote, ikiwemo taarifa kuhusu changamoto za mtoto katika kujifunza na matatizo ya tabia;

(j) hatua za ukuaji; na

(k) taarifa nyingine yoyote muhimu.

Faragha na utunzaji siri

**16.-**(1) Kumbukumbu zote zinazotunzwa na kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga zitatunzwa kwa uangalifu na zitachukuliwa kuwa ni za siri, na zinaweza kutolewa kwa mtu aliyeidhinishwa, ambaye ni-

(a) mfanyakazi ambaye anahitaji taarifa hizo kwa lengo linalohusiana moja kwa moja na majukumu au kazi katika kituo husika cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga;

(b) mzazi au mlezi wa mtoto;

(c) mtu anayefanya upelelezi juu ya malalamiko yaliyofanywa na, au kwa niaba ya mtoto;

(d) kamati ya wazazi;

(e) mtu anayefanya ukaguzi wa kituo husika cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga chini ya mamlaka yaliyotolewa na Sheria, au sheria nyingine yoyote inayohusika;

(f) mtu yeyote aliyepewakibali bayana cha maandishi na Kamishna wa Ustawi wa Jamii;

(g) taasisi yoyote inayotoa elimu ya awali ya msingi au

elimu ya ngazi ya juu.

(2) Kumbukumbu zote kuhusiana na mtoto aliyeandikishwa kwenye kituo husika cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga zitatunzwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Kumbukumbu na Nyaraka.

Ada

**17**.-(1) Kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga kinaweza kutoza ada au malipo mengine kutokana na huduma zinazotolewa na vinavyotolewa kwa mtoto kama Kamishna anavyoweza kuainisha.

(2) Katika kuweka viwango, Kamishna atazingatia-

(a) aina ya kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga kilichopo katika jamii husika;

(b) hitaji la kuzuia upandishaji holela au wa mara kwa mara na usio wa lazima wa ada;

(c) hitaji la kudumisha viwango vya huduma zinazotolewa na kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga;

(d) hitaji la kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kituo cha kulea watoto wachanga na watoto wachanga wasiozidi kumi katika maeneo ya vijijini na mijini;

(e) hitaji la kuhakikisha upatikanaji wa watumishi wa kutosha na wenye sifa kwa ajili ya huduma mbalimbali kwenye kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga; na

(f) hitaji la kuendeleza uwezo wa kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga kuendeleza ufanisi na kupanua huduma zake ili kupokea watoto wengi zaidi.

## SEHEMU YA NNE
### VIWANGO KWA AJILI YA MIUNDOMBINU YA VITUO VYA KULELEA WATOTO WADOGO MCHANA NA WATOTO WACHANGA

Mpangilio wa ujenzi wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na

**18**.-(1) Kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga kitakuwa katika ubunifu, muundo na kitajengwa katika namna inayowezesha kufikiwa kwa urahisi, kukarabatiwa na kuwa salama kwa ustawi wa watoto.

(2) Kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga kitakuwa kwenye eneo linalofaa, ambalo ni salama dhidi

watoto wachanga

ya magari na vitu vingine vyenye madhara.

(3) Iwapo kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga kipo jirani na eneo lenye madhara, barabarani au eneo ambalo lina athari za hali ya juu kiusalama, mipaka ya eneo la kuchezea ni lazima lizungushiwe uzio ndefu.

(4) Madarasa yawe na sakafu ya ukubwa chini wa mita za mraba 1.0 kwa mtoto, bila kujumuisha chumba cha kupumzikia, vyoo, jiko, kumbi, baraza na eneo la kuhifadhia mrefu.

(5) Sakafu zote za zege zinazotumiwa na watoto ni lazima zifunikwe na zulia au kifaa kingine chochote sahihi ili kuzuia madhara kwa watoto.

(6) Kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga na vifaa vyote vilivyo ndani yake vitakuwa na-

(a) nafasi ya kutosha ya kuweka na kuhifadhi vifaa, vyombo na wanasesere kama itakavyokuwa muhimu kwa ajili ya uendeshaji wa kituo husika katika hali ya usafi;

(b) mwanga wa kutosha, madirisha ya hewa vyooni, maeneo ya kunawia mikono, madarasa, na maeneo ambayo chakula kinaandaliwa au kuhifadhiwa na mahali ambapo vifaa na vyombo vinasafishwa;

(c) maji ya kunywa safi na salama na vifaa vya kuhifadhia maji ikitokea dharura;

(d) sakafu, kuta na dari viwe vinavyosafishika, salama kwa watoto na vinatunzwa katika hali nzuri na kukarabatiwa.

(7) Hatua zinazostahili zitachukuliwa ili kuhakikisha kwamba majengo yanafikiwa na watoto wenye mahitaji maalum.

(8) Iwapo majengo yapo kwenye jengo la ghrofa nyingi, madarasa yatapaswa kuwa kwenye ghorofa ya kwanza au ghorofa ya pili ya jengo au kuwa yanafikika moja kwa moja kwa lifti au njia maalum ya kupandia.

(9) Kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga hakitapaswa kuwa na bwawa la kuogelea, na bwawa la kuogelea kwenye kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga litakuwa chini ya usimamizi wa mtu mwenye weledi kwa wakati wote ili kuzuia watoto wasizame.

(10) Pale ambapo kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga wasiozidi kumi kina bwawa la

kuogelea, bwawa hilo litapaswa kuwa limejengwa katika namna inayowezesha kusafishwa kwa urahisi na kutunzwa katika namna nzuri, kuwa salama na kupunguza athari za kuzama.

Usafi wa mazingira

**19.**-(1) Mmiliki yeyote hataanzisha kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga isipokuwa iwapo majengo-

(a) yana maeneo ya kutosha ya kujisaidia na safi kwa matumizi ya watoto, mbali na waajiriwa, ikijumuisha pamoja na vifaa vya kunawia mikono vilivyo karibu na vyoo;

(b) yana vyanzo vya uhakika vya maji; na

(c) yana mfumo sahihi wa majitaka.

(2) Maeneo safi ya kujisaidia katika kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga-

(i) yatapaswa kuwatenganisha watoto na watumishi wengine na wageni;

(ii) yatakuwa tofauti kwa kila jinsi, kundi;

(iii) yatakuwa ni yanayoweza kufikiwa na watoto wenye ulemavu;

(iv) yatatunzwa katika hali safi na nzuri kwa wakati wote;

(v) yataondolewa taka mara kwa mara;

(b) yatakuwa na mabeseni ya kunawia na vyoo vilivyowekwa kulingana na umri wa watoto walioandikishwa;

(c) yatakuwa na milango ya vyooni iliyo katika hali, ukubwa na umbo linalotoa faragha kwa watumiaji wake na rahisi kutumiwa na watoto;

(d) yatapatikana kwa urahisi na kufikika na watoto wenye ulemavu; na

(e) yatawekwa katika hali ya usafi na kutunzwa katika hali nzuri wakati wote; yatakuwa na mfumo salama wa uondoaji taka mara kwa mara.

## SEHEMU YA TANO
### VIFAA VYA KUCHEZEA NA HUDUMA

Wanasesere

**20.**-(1) Mmiliki wa kituo cha kulelea watoto wadogo

mchana au watoto wachanga atahakikisha kwamba kunakuwepo na midoli salama Ya kutosha, na wanasesere wa kuwezesha michezo bunifu, michezo inayochochea ukuaji wa akili kwa ajili ya maendeleo ya kiutambuzi na kumwandaa mtoto kwa ajili elimu ya awali.

(2) Bila ya kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), ya Kanuni hizi kila meneja au mmiliki wa kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga atahakikisha upatikanaji wa vifaa vya michezo, vifaa vya kujifunzia, vifaa saidizi, ambavyo havijatengenezwa au vile ambavyo tayari vimetengenezwa, kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Sita la Kanuni hizi.

Vifaa vya burudani

**21.-**(1) Mmiliki wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga; ataweka na kutunza vifaa salama na vya kutosha kwa ajili ya kuchezea, mahali pa watoto pa kupumzikia, maeneo ya michezo na vifaa vya kuchezea vinavyoendana na umri sahihi wa watoto walioandikishwa.

(2) Meneja au mmiliki wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga ataweka vifaa mbalimbali vya kuchezea vinavoendana na kundi la umri sahihi wa watoto walioandikishwa katika taasisi.

(3) Katika kila kituo cha kulea watoto wachanga au watoto wachanga wasiozidi kumi, kutakuwa na angalu mita za mraba 2.0 za eneo la nje la kuchezea kwa kila mtoto. Eneo lenye chini ya mita za mraba 2.0 kwa mtoto linaweza kuruhusiwa baada ya kuwasilishwa ushahidi kwa afisa muidhinishwa wa uwekwaji wa vifaa kwa umakini na ukomo wa matumizi ya vifaa kwa makundi madogo kwa wakati mmoja.

(4) Vifaa vya kuchezea na maeneo yake yatapaswa kuwa salama ili kupunguza athari za madhara kwa watoto.

Chakula na lishe

**22.-**(1) Pale ambapo kituo chochote cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga kinatoa huduma ya chakula, mmiliki atahakikisha kwamba:

(a) chakula kinatolewa kwa kiwango kinachotakiwa na kina ubora unaoendana na mahitaji ya watoto walio katika kituo husika. Hii itawezekana kwa kufanya mashauriano na wataalamu wa lishe, na pia itatafsiriwa kwenye miongozo;

(b) mlo unatolewa kwa vipindi mahsusi na nyakati ambazo ni sahihi kulingana na umri wa mtoto;

(c) mahitaji yoyote ya mahsusi wa mtoto kutokana na sababu za kiafya au kidini yanazingatiwa;

(d) maziwa yanayotolewa kwa watoto yanaendana na umri wa mtoto na yanakidhi taratibu za mauzo ya Maziwa Mbadala ya Kunyonyesha;

(e) chumvi yenye madini chuma pekee ndiyo inayotumiwa kwenye vyakula;

(f) chakula kinahifadhiwa ipasavyo mahali safi ili kuzuia maambukizi na milipuko ya magonjwa; na

(g) maji safi na salama yanapatikana kwa watoto na kwa wakati wote.

(2) Mmiliki au meneja wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga atahakikisha kwamba mahali panapotumiwa kwa ajili ya maandalizi na kula chakula ni safi wakati wote na inaendana na umri wa watoto walioandikishwa.

(3) Mmiliki wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga atahakikisha kwamba jiko linapata maji safi na salama.

(4) Meneja au mmiliki wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga atahakikisha kwamba mtu mwenye ujuzi na weledi wa masuala ya lishe ameajiriwa kwenye kituo husika.

Vifaa kwa watoto walio chini ya miaka miwili

**23.** Mtu hatamwandikisha mtoto wa chini ya umri wa miaka miwili isipokuwa kama yafuatayo yanapatikana:

(a) mahali salama pa kubadilishia nepi;

(b) taulo za kufutia au nepi zinazotumika na kutupwa;

(c) vifaa safi vya kujisaidia watoto ambavyo vinahimiza matumizi ya kujitegemea ya choo kwa uwiano wa 1:5 wa watoto;

(d) sehemu tofauti ya kusafishia poti za watoto;

(e) vifaa vya kutunzia nepi chafu; na

(f) kitanda kimoja kisafi na godoro au zulia safi kwa kila mtoto ambaye anatumia zaidi ya saa nne kwa siku katika taasisi, kukiwa na nafasi ya angalau futi mbili kati ya kila zulia au godoro.

Usalama

**24**. Mmiliki au meneja atahakikisha kwamba-
(a) jiko halifikiwi kiurahisi na watoto;
(b) kuna vifaa vya kuzimia moto vinavyofanya kazi na vinavyofikika iwapo moto utatokea;
(c) kuna kisanduku cha huduma ya kwanza kilichohifadhiwa mahali pasipoweza kufikiwa na watoto, kikiwa na madawa ya kutosha, ambayo yanapaswa kuhakikiwa na kubadilishwa mara kwa mara na mtumishi mwenye ujuzi wa huduma ya kwanza; na
(d) kuna mpango mahsusi wa rufaa iwapo kutatokea dharura za kimatibabu ambazo zinafahamika kwa watumishi wote na pia kuna mawasiliano na zahanati au hospitali za jirani iwapo kutatokea ajali au ugonjwa.

## SEHEMU YA SITA
### UKAGUZI

Ukaguzi wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga

**25.-**(1) Vituo vyote vya kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga vitatakiwa kufanyiwa ukaguzi kama ilivyowekwa kwenye Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

(2) Kamishna atahakikisha kwamba ukaguzi wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga unafanyika angalau mara moja katika kila miezi sita.

(3) Ukaguzi unaorejewa kwenye kanuni ndogo ya (1) utatekelezwa na Afisa Ustawi wa Jamii katika ngazi ya mamlaka ya serikali ya mtaa.

(4) Mkaguzi wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga ataandaa na kuwasilisha taarifa ya ukaguzi katika namna iliyowekwa kwenye Jedwali la Saba la Kanuni hizi na nakala ya taarifa hiyo itapelekwa kwa mmiliki wa kituo husika cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga.

(5) Ikitokea kwamba kituo husika cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga kipo chini ya viwango vinavyotakiwa na Kanuni hizi, taarifa itajumuisha maelekezo ya hatua ambazo mmiliki anapaswa kuchukua ili kukidhi viwango husika.

(6) Kamishna atatoa muda usiopungua miezi miwili na usiozidi miezi sita kwa mmiliki kutekeleza maelekezo yaliyo kwenye taarifa ya ukaguzi.

(7) Afisa Ustawi wa Jamii atatathmini iwapo au la, maelekezo ya maboresho katika taarifa ya kwanza yametekelezwa.

(8) Kamishna anaweza kufuta cheti cha usajili iwapo mwenye usajili anashindwa kutekeleza maelekezo yaliyotolewa kwenye taarifa ya ukaguzi.

(9) Pale ambapo Kamishna atafuta usajili, mwenye usajili anaweza kukata rufaa kwa Waziri ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kutolewa uamuzi.

(10) Waziri atatoa nafasi ya kusikilizwa kwa mwenye usajili kabla ya kutoa uamuzi kuhusu rufaa chini ya kanuni ndogo ya (9).

(11) Waziri atatafakari rufaa na kutoa uamuzi wake ndani ya siku arobaini na tano toka tarehe ya kupokea rufaa husika.

## SEHEMU YA SABA
### MASHARTI YA JUMLA

Rejesta ya vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na watoto wachanga

**26.-**(1) Kila kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga kitaanzisha na kutunza rejesta itakayokuwa na taarifa zifuatazo:

(a) jina la mwenye usajili;
(b) jina la kituo husika cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga;
(c) namba ya cheti cha usajili;
(d) wilaya;
(e) kata;
(f) uwezo wa kituo husika;
(g) jinsi ya mtoto; na
(h) iwapo au la, taasisi ina vifaa vinavyohitajika kwa watoto wenye mahitaji maalum na wale wenye ulemavu.

(2) Kamishna ataanzisha na kutunza rejesta ya Taifa ya vituo vyote vya kulea watoto wachanga au watoto wachanga wasiozidi kumi katika namna iiliyoainishwa kwenye Fomu Na. 4 katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

(3) Afisa Ustawi wa Jamii ataanzisha na kutunza rejesta ya Wilaya ya vituo vyote vya kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga katika namna iliyowekwa kwenye Fomu Na. 4 katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

Taarifa za robo mwaka na za mwaka mzima

**27**.-(1) Kila mmiliki wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga atawasilisha taarifa ya robo mwaka na taarifa ya mwaka kwa Afisa Ustawi wa Jamii katika fomu iliyoainishwa kwenye Jedwali la Nane.

(2) Afisa Ustawi wa Jamii atawasilisha taarifa zilizorejewa katika kanuni ndogo ya (1) kwa Kamishna ndani ya siku saba tangu tarehe ya kupokea taarifa hiz,o, kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto na Kanuni zake.

Muda wa kufungua vituo vya kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga

**28**.-(1) Kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga hakitafanya kazi-

(a) kwa zaidi ya masaa kumi kwa siku; na

(b) kati ya saa 2 usiku na saa 12 asubuhi.

(2) Iwapo kituo cha kulea watoto wachanga au watoto wachanga wasiozidi kumi kinafanya kazi kwa zaidi ya saa sita, mmiliki wake atahakikisha kwamba kituo hicho kina malazi safi ili kuruhusu watoto kujipumzisha.

(3) Makao ya za watoto au shule za watoto wenye mahitaji maalum zinaweza kuendesha vituo vya kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga;iwapo nyumba hizo za watoto au shule za watoto wenye mahitaji maalum zimekidhi masharti yote ya nyumba za watoto na pia vituo vya kulea watoto wachanga na watoto wachanga wasiozidi kumi.

Vituo vya kulelea watoto wadogo mchana vya jamii

**29**.-(1) Kamishna anaweza kuondoa matumizi ya masharti yoyote ya Kanuni hizi kwa kituo chochote cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga kinachomilikiwa na jamii.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1), Kamishna atatoa miongozo kuhusu masharti yatayoondolewa, na kwa ajili ya uendeshaji, usimamizi na uangalizi wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga vya jamii.

Kufutwa kwa Kanuni T.L Na. 108 la mwaka 1982

**30**. Kanuni za Vituo vya kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga za mwaka 1982 zinafutwa.

## MAJEDWALI

**JEDWALI LA KWANZA**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

**D.C.C Fomu Na. 1**

MAOMBI YA USAJILI WA KITUO CHA KULELEA WATOTO WADOGO MCHANA AU WATOTO WACHANGA

Kwa Afisa Ustawi wa Jamii

………………………….

……………………….

Mimi/Sisi* tunaomba usajili wa Kituo changu/chetu* kilichopo/kipya* cha kulelea watoto wadogo mchana kwa mujibu wa Sheria ya

Mtoto na kanuni zilizotengenezwa chini yake kama ifuatavyo:

Jina la Mwombaji/Waombaji………………………………………………………………………

Anwani ya mahali anapoishi………………………… Namba ya Simu…………………………..

Namba ya simu ya kiganjani………………………… Anwani ya barua pepe…………………….

Kazi………………………………………………………………………………………………

Uraia Mtanzania [ ] Raia wan chi nyingine [ ]

Aina ya maombi Peke yangu [ ] Pamoja na raia wa Tanzania [ ]

Mahali/ Anwani ya Eneo kituo kilipo………………………………………………………….....

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

Idadi ya juu ya watoto **walioandikishwa/wanaokusudiwa*** kuandikishwa kwenye Kituo cha kulelea watoto wadogo mchana …………

Idadi ya juu ya watoto chini ya miaka miwili **walioandikishwa/wanaokusudiwa*** kuandikishwa kwenye kulelea watoto wadogo mchana …………

Idadi ya juu ya watoto wenye miaka 2-5 **walioandikishwa/wanaokusudiwa*** kuandikishwa kwenye Kituo cha kulelea watoto wadogo mchana …………

**Mimi/Sisi* tunakusudia/hatukusudii*** kuandikisha watoto wenye ulemavu na/au wenye mahitaji maalum kwenye Kituo cha

Kulelea watoto wadogo mchana.

**TAMKO**

Mimi/Sisi tunakiri kwamba taarifa zilizotolewa hapo juu ni za kweli kulingana na uthabiti wa uelewa wangu/wetu* na iwapo

itabainika kwamba taarifa hizo ni za uongo na zimetolewa kwa makusudi maombi yangu/yetu* yatupiliwe mbali.

Sahihi ya/za Mwombaji/Waombaji…………………………………………………………………

**<u>Kwa matumizi ya kiofisi ya Afisa Afya</u>**

Ninathibitisha kwamba nimekagua majengo husika na nimejiridhisha/sijajiridhisha* kwamba majengo hayo yanafaa/hayafai*

kwa uendeshaji wa Kituo cha Kulelea Watoto wadogo mchana.

Iwapo majengo hayafai, toa sababu za tathmini hii:

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

Tarehe………………………………. Jina na wadhifa………………………………………………

Sahihi………………………………………………………

**<u>Kwa matumizi ya kiofisi ya Afisa Ustawi wa Jamii</u>**

Ninathibitisha kwamba mwombaji/waombaji wametimiza mahitaji ya kuendesha Kituo cha Kulelea Watoto wadogo mchana na

wanastahili/hawastahili* kusajiliwa kuendesha Kituo Kidogo cha Kulea Watoto Wachanga.

Idadi ya juu ya watoto wanaoweza kuhudhuria kwenye Kituo cha Kulelea watoto wadogo mchana ni ……………………..
Idadi ya juu ya watoto chini ya miaka miwili walioruhusiwa kuandikishwa kwenye Kituo cha Kulelea watoto wadogo mchana ni …………...........
Idadi ya juu ya watoto wa 2-5 walioruhusiwa kuandikishwa kwenye Kituo cha Kulelea Watoto wadogo mchana ……….....…

Iwapo mwombaji/waombaji hafai, maombi yake yamekataliwa/yamerudishwa*. Elezea sababu za kukataa au hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kukidhi masharti ya Kanuni hizi iwapo maombi yamerudishwa.

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
……………………………,,,,…………………………………………………………………

Tarehe…………………………… Jina na wadhifa ………………………………………………

Sahihi…………………………………………………….

* *futa kisichohusika*

**D.C.C Fomu Na. 2**

MAOMBI YA KUSAJILI KITUO CHA KULELEA WATOTO WACHANGA

*(Yamefanyika chini ya kanuni ya 4(1))*

_____

Kwa Afisa Ustawi wa Jamii

………………………….

……………………….

Mimi/Sisi* tunaomba usajili wa Kituo Kidogo changu/chetu* kilichopo/kipya* cha Kulelea a Watoto wachanga kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto na kanuni zilizotengenezwa chini yake kama ifuatavyo:

Jina la Mwombaji/Waombaji……………………………………………………………………

Anwani ya mahali anapoishi………………………… Namba ya Simu…………………………..

Namba ya simu ya kiganjani………………………… Anwani ya barua pepe…………………….

Kazi………………………………………………………………………………………………

Uraia Mtanzania [ ] Raia wan chi nyingine [ ]

Aina ya maombi Peke yangu [ ] Pamoja na raia wa Tanzania [ ]

Mahali/ Anwani ya Eneo kituo kilipo………………………………………………………....

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

Idadi ya juu ya watoto **walioandikishwa/wanaokusudiwa*** kuandikishwa kwenye Kituo Kidogo cha Kulelea watoto wachanga.

Idadi ya juu ya watoto chini ya miaka miwili **walioandikishwa/wanaokusudiwa*** kuandikishwa kwenye Kituo Kidogo cha kulelea watoto wachanga…………………………

Idadi ya juu ya watoto wenye miaka 2-5 **walioandikishwa/wanaokusudiwa*** kuandikishwa kwenye Kituo Kidogo cha kulelea watoto wachanga…………………………

**Mimi/Sisi* tunakusudia/hatukusudii*** kuandikisha watoto wenye ulemavu na/au wenye mahitaji maalum kwenye Kituo kidogo cha kulelea watoto wachanga.

**TAMKO**

Mimi/Sisi tunakiri kwamba taarifa zilizotolewa hapo juu ni za kweli kulingana na uthabiti wa uelewa wangu/wetu* na iwapo

itabainika kwamba taarifa hizo ni za uongo na zimetolewa kwa makusudi maombi yangu/yetu* yatupiliwe mbali.

Sahihi ya/za Mwombaji/Waombaji…………………………………………………………………

**<u>Kwa matumizi ya kiofisi ya Afisa Afya</u>**

Ninathibitisha kwamba nimekagua majengo husika na nimejiridhisha/sijajiridhisha* kwamba majengo hayo yanafaa/hayafai*

kwa uendeshaji wa Kituo cha kulelea watoto wachanga.

Iwapo majengo hayafai, toa sababu za tathmini hii:

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

Tarehe……………………………. Jina na wadhifa…………………………………………………

Sahihi……………………………………………………

**<u>Kwa matumizi ya kiofisi ya Afisa Ustawi wa Jamii</u>**

Ninathibitisha kwamba mwombaji/waombaji wametimiza mahitaji ya kuendesha Kituo cha Kulelea Watoto wachanga **wanastahili/hawastahili*** kusajiliwa kuendesha Kituo cha kulelea watoto wachanga.

Idadi ya juu ya watoto wanaoweza kuhudhuria kwenye Kituo cha Kulea Watoto wachanga wasiozidi kumi ni ……………………..
Idadi ya juu ya watoto chini ya miaka miwili walioruhusiwa kuandikishwa kwenye Kituo cha Kulelea Watoto wachanga …………..........................
Idadi ya juu ya watoto wa 2-5 walioruhusiwa kuandikishwa kwenye Kituo Kidogo cha Kulea Watoto Wachanga ………….....

Iwapo mwombaji/waombaji hafai, maombi yake yamekataliwa/yamerudishwa*. Elezea sababu za kukataa au hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kukidhi masharti ya Kanuni hizi iwapo maombi yamerudishwa.

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………

Tarehe…………………………… Jina na wadhifa ………………………………………………

Sahihi…………………………………………………….

* *futa kisichohusika*

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(5))*

**D.C.C Fomu Na. 3**

CHETI CHA USAJILI WA KITUO CHA KULELEA WATOTO WADOGO MCHANA NA WATOTO WACHANGA

Hii ni kuthibitisha kwamba …………………………………………………………………

(Jina la Mwombaji/Waombaji)

Kutokana na maombi ya cheti cha kuendesha Kituo cha Kulelea Watoto wadogo mchana/Watoto Wachanga * na kwa kukidhi vigezo, baada ya ukaguzi, vilivyowekwa chini ya Sheria ya Mtoto na Kanuni zilizotengenezwa chini yake, anapewa usajili wa kuendesha Kituo cha Kulelea Watoto Wadogo mchana/Watoto Wachanga:

Wilaya:……………………………..…………………..
Kata:……………………………………………………

na Kituo hicho cha Kulelea Watoto watoto wadogo mchana /Watoto Wachanga kitajulikana kama:

…………………………………………………………………………………………………….

Kikiwa na Namba ya Usajili:

………………………………………………………………………………………

Kimetolewa na:

Sahihi:…………………………………………………………………………………………………

Kamishna wa Ustawi wa Jamii:

Mahali:………………………………….. Tarehe:……………………………………………

* *futa kisichohusika*

Idadi ya Waangalizi:

| **Sifa** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Shahada | | | |
| Stashahada | | | |
| Cheti cha ustawi wa jamii au malezi ya watoto | | | |

Majina na nyadhifa za waajiriwa wengine wote……………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

Je, watoto hupewa chakula? Ndio/Hapana

Kama jibu ni Ndio, taja mtoaji wa chakula hicho…………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

Kama jibu ni Hapana, toa sababu………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………………

………………… ……………………………………………

**Tarehe** **Sahihi ya Meneja/Mmiliki wa Kituo cha Kulea Watoto Wachanga/Watoto Wachanga Wasiozidi Kumi**

**D.C.C Fomu Na. 4**

REJESTA YA KITUO CHA KULELEA WATOTO WADOGO MCHANA NA WATOTO WACHANGA

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 25(1))*

______

| Namba ya usajili | Jina la kituo cha kulelea watoto wadogo mchana/kituo cha watoto wachanga | Jina la Kituo/Kituo Kidogo | Wilaya | Kata | Idadi ya juu ya uwezo wa kituo cha watoto kulelea watoto wadogo mchana /kituo cha kulea watoto wachanga ` | | | Jinsi ya watoto (ainisha iwapo kituo kinaandikisha wavulana (M) au wasichana (F) au wavulana na wasichana kwa pamoja (M/F) | Ainisha iwapo kituo kinaandikisha watoto wenye mahitaji maalum na/au wenye ulemavu (andika NDIO au HAPANA) | Tarehe ya kwanza ya Idhini |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Miaka 0 hadi 2 | Miaka 2 hadi 5 | Jumla | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |

**JEDWALI LA TATU**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7(1))*

MUUNDO WA KAMATI YA WAZAZI

| | |
|---|---|
| Mwenyekiti: | Atachaguliwa kutoka miongoni mwa wazazi. |
| Katibu: | Mtumishi mwangalizi wa mtoto. |
| Wajumbe wanne: | Watachaguliwa na wazazi kutoka miongoni mwa wazazi. |

Maafisa wafuatao kutoka ngazi ya Kata wataalikwa:

Afisa Afya

Asasi isiyo ya Kiserikali inayojihusisha na watoto

Afisa Maendeleo ya Jamii

Afisa Elimu

______

**JEDWALI LA NNE**

______

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 12(4))*

________

IDADI YA CHINI YA WATUMISHI WAANGALIZI WA ZAMU/UWIANO WA MTOTO

**Idadi ya chini ya waangalizi wa mtoto/uwiano wa mtoto**

Chini ya miaka 2 – 1:10
Miaka 2-5 – 1:20

Bila kujali uwiano ulioainishwa hapo juu, si chini ya mwangalizi mmoja anapaswa kuwa zamum kwa muda wote wakati wa masaa ya kazi ya kituo cha kulelea watoto wadogo mchana na watoto wachanga.

**Uwezo wa juu wa kila mwangalizi**

Bila kujali uwiano ulioainishwa kwenye Jedwali hili, mmiliki au meneja ni lazima ahakikishe kwamba watumishi waangalizi wa kutosha wapo zamu wakati wa masaa ya kazi ya kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga ili kuhakikisha kwamba hakuna mtumishi mwangalizi anawajibika peke yake kwa watoto zaidi ya 15.

______

**JEDWALI LA TANO**

______

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 13)*

______

KANUNI ZA MAADILI YA ……………………………………………….

Mimi, Jina ………………………………….. Cheo ………………………………………. Nakubali kudumisha kiwango cha hali ya juu cha viwango vya watumishi na mienendo ya kiweledi kwa nyakati zote katika kuchangamana kwangu kote na watoto:

(1) Nitawalinda na kuwatunza watoto dhidi ya aina zote za vurugu, udhalilishaji, unyanyasaji, madhara au kutelekezwa;

(2) Nitachangamana na watoto kwa heshima bila kujali rangi, jinsi, lugha, hali ya kisiasa au nyingineyo, utaifa, kabil au asili ya kijamii, mali, ulemavu, hali ya kiafya, kuzaliwa au hali nyingineyo;

(3) Sitawabagua, kuwatendea kwa utofauti au kupendelea aina Fulani ya watoto na kuwatenga wengine;

(4) Sitatumia lugha au tabia ambayo si sahihi, inayodhalilisha, yenye matusi, yenye viashiria vya ngono au isiyo sahihi kiutamaduni kwa watoto;

(5) Nitaheshimu usafi wa mwonekano wa watoto wote;

(6) Sitawahusisha watoto kwenye shughuli zozote au vitendo vya ngono, ikiwa ni pamoja na kuwalipa kwa ajili ya huduma au vitendo vya ngono;

(7) Sitaonesha tabia ya kimwili katika namna isiyofaa au inayochochea ngono, au kuonesha tabia isiyofaa au uhusiano wa aina yoyote;

(8) Sitatenda jambo lolote katika namna inayoweza kuleta aibu, kunyanyapaa, kudhalilisha au kuwashushia heshima watoto au kuonesha aina yoyote ya udhalilishaji wa kihisia;

(9) Sitajihusisha na aina yoyote ya unyanyasaji wa watoto au kuwaweka watoto katika hali ambayo itawaweka kwenye hatari ya aina yoyote ya unyanyasaji;

(10) Sitaanzisha uhusiano na watoto ambao kwa namna yoyote ile unaweza kuchukuliwa kuwa ni wa kinyanyasaji au unaodhalilisha au kutenda jambo kwa namna yoyote ambayo inaweza kumweka mtoto kwenye hatari ya kudhalilishwa;

(11) Sitapuuza au kushiriki kwenye tabia isiyo halali kisheria, isiyo salama au inayodhalilisha watoto;

(12) Nitajiepusha kuangalia, kumiliki, kuandaa au kusambaza picha za ngono za watoto;

(13) Nitaheshimu faragha ya watoto na sitampiga mtoto picha ya mnato au video bila ridhaa zao na ridhaa ya meneja;

(14) Sitamwalika nyumbani kwangu mtoto peke yake, isipokuwa iwapo wapo kwenye uwezekano wa kupata hatari dhahiri ya majeraha au wapo hatarini kwelikweli;

(15) Sitawakodisha watoto kwa ajili ya kufanya kazi za nyumbani au za aina nyingine ambazo si sahihi kulingana na umri wao au hatua yao ya ukuaji, ambazo pia zinaingiliana na muda wao wa masomo na wa maburudisho, au ambazo zinawaweka katika hatari dhahiri ya madhara;

(16) Nitatii sheria zote husika za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikiwemo sheria zinazohusiana na ajira ya mtoto; na

(17) Nitatoa taarifa mara moja kuhusiana na suala au tuhuma inayohusiana na ukatili yoyote, udhalilishaji au unyanyasaji wa mtoto kwa mujibu wa taratibu sahihi.

Naelewa kwamba wajibu ni wangu kutumia akili ya kawaida na kuacha vitendo au tabia ambazo zinaweza kutafsiriwa kuwa ni za kudhalilisha, zinazonyanyasa au kuleta madhara kwa watoto.

Sahihi: …………………………………………………….
Tarehe:………………………………..

**JEDWALI LA SITA**

(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 20(2))

WANASESERE, VIFAA NA VITU VINAVYOPASWA KUTOLEWA KATIKA KULELEA WATOTO WADOGO MCHANA

**A. Vifaa vya Kituo cha kulelea watoto wadogo mchana:**

Meza na viti vya waajiriwa, meza ndogo na viti vya watoto.
Mazulia
Ubao
Kabati au shelfu la kuhifadhia vifaa
Vitanda/malazi kwa watoto walio kwenye kituo
Kisanduku cha huduma ya kwanza

**B. Vyombo vya jikoni:**

Vyombo vya kupikia na kulia chakula
Vyombo vya kubebea na kuhifadhia maji
Nguo za jikoni
Kabati la kuhifadhia vyombo

**C. Vifaa vya michezo na burudani**

**D. Michezo ya ndani**

---

**JEDWALI LA SABA**

---

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 25(4))*

---

TAARIFA YA TATHMINI NA UKAGUZI

1. Jina la Kituo cha Kulelea Watoto Wadogo …………………………………..
2. Namba ya usajili ya Kituo cha Kulelea Watoto Wadogo mchana ………………………..
3. Jina/Majina ya meneja/mameneja au mmiliki/wamiliki…………………………………..
4. Asili ya umiliki **BINAFSI/UBIA/UMMA***
5. Uraia wa mmiliki/wamiliki au meneja/mameneja **MTANZANIA/RAIA WA KIGENI/VYOTE VIWILI**
6. Mahali Kituo cha Kulelea Watoto Wadogo mchana kilipo:

   Wilaya:…………………………………….. Kata……………………………………….

   Mtaa:……………………………………………………….

   Anwani ya Posta: …………………………………………….

   Simu ya mezani: ………………………………………………..

   Simu ya mkononi: …………………………………………………..

   Barua pepe: ……………………………………………………….
7. Idadi ya juu ya watoto walio kwenye Kituo cha Kulelea Watoto Wadogo mchana (wavulana na wasichana)….
8. **(a) Taarifa za watoto kwenye Kituo cha Kulea Watoto Wachanga**

| **UMRI** | **WASICHANA** | **WAVULANA** | **JUMLA** |
|---|---|---|---|
| Chini ya umri wa miaka 2 | | | |
| Miaka 2-5 | | | |

**(b) Taarifa za watoto wenye mahitaji maalum**

| **UMRI** | **WASICHANA** | **WAVULANA** | **JUMLA** |
|---|---|---|---|
| Chini ya miaka 2 | | | |
| Miaka 2-5 | | | |

Maelezo ya tathmini

| | | |
|---|---|---|
| 9. | Je kuna kamati ya wazazi? | **NDIO/HAPANA*** |
| 10. | Je muundo wa kamati ya wazazi unaendana na kanuni hizi? | **NDIO/HAPANA*** |
| 11. | Je, kuna taratibu zozote za usalama wa mtoto? | **NDIO/HAPANA*** |
| 12. | Je, watumishi waangalizi/uwiano wa mtoto upo sambamba na Kanuni hizi? | **NDIO/HAPANA*** |
| 12a | Kama jibu ni HAPANA, ni sababu zipi zimesababisha kutotekelezwa huko? | |
| 13. | Je, watumishi waangalizi wa mtoto wana sifa zilizoainishwa kwenye kanuni hizi? | **NDIO/HAPANA*** |
| 13a | Kama jibu ni HAPANA, ni sababu zipi zimesababisha kutotekelezwa huko? | |
| 14. | Je, kuna watoto wenye ulemavu, maradhi sugu au wenye HIV/AIDS? | **NDIO/HAPANA*** |
| 14a | Kama jibu ni NDIO, Je meneja/mameneja au mmiliki/wamiliki wameweka mazingira wezeshi kwa kuzingatia kanuni hizi? | **NDIO/HAPANA*** |
| 15. | Je, wajumbe wa kamati ya wazazi, watumishi na wadau wengine wamesaini Kanuni za Maadili? | **NDIO/HAPANA*** |
| 15a | Kama jibu ni HAPANA, ni sababu zipi zimesababisha kutotekelezwa huko? | |
| 16. | Je, kuna mfumo sahihi wa kutunza kumbukumbu? | **NDIO/HAPANA*** |

| | | |
|---|---|---|
| 16a | Kama jibu ni HAPANA, ni sababu zipi zimesababisha kutotekelezwa huko? | |
| 17. | Je, kuna jalada binafsi kwa kila mtoto aliye kwenye kituo au kituo kidogo? | **NDIO/HAPANA*** |
| 17a | Kama jibu ni HAPANA, ni sababu zipi zimesababisha kutotekelezwa huko? | |
| 18. | Je, majengo yamewekwa katika hali safi na ya kiafya? | **NDIO/HAPANA*** |
| 19. | Je, majengo yanafaa kwa ajili ya kituo cha kulelea watoto wadogo mchana/watoto wachanga? | **NDIO/HAPANA*** |
| 20. | Je, vifaa vyote muhimu vipo? | **NDIO/HAPANA*** |
| 20a | Kama jibu ni HAPANA, ni kitu gani kimekosekana na kwa nini? | |
| 21. | Je, kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga kinatoa huduma ya chakula? | **NDIO/HAPANA*** |
| 21a | Kama jibu ni NDIO, je chakula kinachotolewa kinatolewa kwa kiasi cha kutosha, kinaandaliwa vizuri na kina virutubisho stahiki? | **NDIO/HAPANA*** |
| 21b | Kama jibu ni HAPANA, ni mapungufu gani au matatizo yaliyobainika? | |
| 22. | Je, kituo au kituo kidogo cha kulea watoto wachanga au watoto wachanga wasiozidi kumi kinafaa na ni salama kwa watoto? | **NDIO/HAPANA*** |
| 22a | Kama jibu ni HAPANA, nini udhaifu/matatizo yake? | |
| 23. | Taja tarehe ya mwisho ambapo ukaguzi ulifanyika. | |
| 23a | Je, kuna hatua zilizochukuliwa kukidhi maelekezo yaliyotolewa kwenye ukaguzi uliopita? (jibu N/A iwapo huu ni ukaguzi wa kwanza) | **NDIO/HAPANA/N/A*** |
| 23b | Toa maelezo kuhusu hatua zilizochukuliwa kutekeleza maelekezo na melezo ya maelekezo ambayo hayajafanyiwa kazi: | |

24. Toa melezo mengine yoyote stahiki…………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………..

25. Muhtasari wa tathmini

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………….

Mapendekezo

Ninathibitisha kwamba nimetathmini na kukagua kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga hapo juu na kwamba NINAPENDEKEZA yafuatayo:…………………………………………………

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

Sahihi:……………………………………… Tarehe: …………………………………

Jina: ………………………………………………. Wadhifa: ………………………

Cheo:…………………………………………………………………………………..

______

**JEDWALI LA NANE**

________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 27)*

_____

TAARIFA YA ROBO MWAKA

Jina la Kituo cha Kulelea Watoto wadogo mchana au watoto wachanga ………………..

Anwani ya Kituo cha Kulelea Watoto wadogo mchana au watoto wachanga …………. ………………………………………………………………………………………………… …………………………..…………………………………………………………………….

Jina la Mmiliki/Meneja ………………...…………………………………………………..

Namba ya usajili ………………………….……………………………………………..

Idadi ya watoto walioandikishwa kwenye Kituo cha Kulelea Watoto wadogo mchana au watoto wachanga …………………….......

| Umri wa watoto walioandikishwa | Wavulana | Wasichana | Watoto wenye mahitaji maalum | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Chini ya miaka 2 | | | | |
| Miaka 2-5 | | | | |

Wastani wa mahudhurio ya kila siku [iwapo hii ni taarifa ya robo] ……………………………..

Wastani wa mahudhurio ya mwezi [iwapo hii ni taarifa ya mwaka] ………………………………

**Watumishi**

Idadi ya watumishi waangalizi wa mtoto katika Kituo cha Kulea Watoto wachanga/watoto wachanga ………………..

Idadi ya Wafanyakazi waangalizi wa mtoto ………………………………………….

Idadi ya watoa uangalizi …………………………………………………

| Sifa | Wanaume | Wanawake | Jumla |
|---|---|---|---|
| Shahada | | | |
| Stashahada | | | |
| Cheti cha maendeleo ya jamii au malezi ya mtoto | | | |

Majina na nyadhifa za waajiriwa wengine wote ………………………………………...

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………….....

Je, watoto hupewa chakula? Ndio/Hapana

Kama jibu ni Ndio, taja jina la msambazaji wa chakula …………………………………..

………………………………………………………………………………………..

Kama jibu ni hapana, toa sababu……………………………………………………….

……………………………………………………………………………………….

………………………                ……………………………..................

Tarehe                Saini ya Meneja/Mmiliki wa Kituo
Kituo cha kulelea Watoto wadogo mchana/Watoto wachanga

Dar es Salaam,                SEIF SELEMAN RASHID,
............................, 2014                *Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii*